

# KUKUMBATIA KIMUNGU

## *Na Francois du Toit*

*©Hakimiliki 2010*

*(Unahimizwa kusambaza kwa uhuru - tazama ukurasa wa mwisho kwa maelezo)*

mirrorWORD

## UTANGULIZI NA Kobus Grove

“Maana wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu, uliniunga tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendoyako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana; mifupa yangu haikusitirika kwako, nilipoumbwa kwa siri, nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi. *Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; chuoni mwako ziliandikwa zote pia, siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado.* Mungu, fikira zako zina thamani nyingi kwangu; Jinsi ilivyo kubwa jumla yake! Kama ningezihesabu ni nyingi kuliko mchanga; Niamkapo nikalipamoja nawe.” Zab. 139:13-18. REB.

Nilipotambua jinsi nilivyo wa thamani kwa Mungu, na kwamba andiko la hapo juu lina ukweli, kila mtu alifanyika kuwa wa thamani kwangu. Kwa hiyo, ombi langu ni kuwa unaposoma kitabu hiki, uweze kufikia kutambua kikamilifu jinsi ulivyo wa thamani kwa Mungu, na ufahamu kamili wa utambulisho wako wa kweli katika YesuKristo. Ninyi ni wana na binti wa Mungu. Ulikufa pamoja naye msalabani, na ulifufuliwa pamoja naye kutoka kwa wafu. Kwa njia ya utii wa Kristo aliyeutoa mwiliwake mara moja kwa ajili ya wote; hivi sasa tumetangaziwa kuwa wenye haki kwa imani. Hatuna lawama na bila hatia mbele ya macho yake, na tuko huru kufurahia bila kuingiliwa, uhusiano wa ndani pamoja na Mungu kwa maisha yetu yote! “Katikamapenzi hayo tumepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu kristo mara moja tu.”Ebr. 10:10. Haoni haya kutuita sisi ndugu zake, kwa kuwa,”Yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja.” Ebr. 2:2. Ni kutoka kwake sisitunapata asili yetu, kwa njia ya Yesu Kristo ambaye Mungu alimtoa kuwa hekima yetu, haki yetu, utakaso wetu na ukombozi. 1Kor. 1:30. Tafsiri ya Knox.





## MFANO MTAKATIFU

Kiini kikuu na ufunuo wa Biblia unafurahia uhusiano uliopo kati ya Mungu na na mwanadamu ulio wa hali ya juu, muunganiko wa uadilifu kabisa, usio na hali yoyoteya kutengana, kujiona duni, hatia, hukumu au shuku. Muda mtakatifu , wakati kwa mara ya kwanza katika historia ya dunia, Muumba asiyeonekana aliakisi mfano wakena sura yake katika vyombo dhaifu vya mwili, na kufanyika utukufu wa uwepo na kusudi lake duniani, ambalo lingetawala historia ya mwanadamu na hatima yao. Mwanzo 1:26,27,31. Ufunuo wa Injili unaonyesha jinsi Mungu alivyohifadhi chapa yakusudi la kuwepo kwetu katika Kristo ijapokuwa mwanadamu alianguka katika dhambi. Ushirika wetu wa milele katika Kristo tangu kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu, tulikombolewa. Ef. 1:4,5. Mungu alitupata katika Kristo kabla ya kutupoteza katika Adamu! Kuna jambo kubwa lililofanywa na anguko la Adamu, wakati maana iliyo kubwa zaidi imetupa kustahili tazamio letu lisilobadilika. Yoh. 10:10. Ujumbe wa upatanisho unasisitiza ubunifu ambao Mungu aliufanya, na unafunua jinsi Mungu alivyofanikiwa kumrejesha kwake mwanadamu aliyeanguka na kuwa bila hatia kabisa. 1Kor. 1:30; 2Kor. 5:18,19; Rum. 1:16,17; 5:12-20. .

Mwanadamu yupo ili kuwa na muunganiko na Muumba wake, katika uumbaji wake, naye ni mfano wa Mungu, aliumbwa kwa ajili ya ushirikiano mtakatifu na kuonana. Mwanadamu ni ndoto ya upendo wa Mungu. Ef. 1:4,5. “Mimi nimesema, Ndinyi miungu, na wana wa Aliye juu. Lakini mtakufa kama wanadamu.” Zab. 82:6,7. “Humkumbuki Mwamba aliyekuzaa, Mungu aliyekuzaa umemsahau.” Kumb. 32:18.Katika Zaburi 22, Daudi anatabiri kifo cha Masihi Kristo, na anaona matokeo

ya ushindi katika msitari wa 27, "Miisho yote ya dunia itakumbuka, na watu watamrejea BWANA; Jamaa zote za mataifa watamsujudia!" Ndani ya Kristo, Mungu alishughulika na kila udhuru uwezekanao ambao mtu angekuwa nao na kujihisi kutengwa mbali na Mungu; Yeye ni njia kuu jangwani aliyoiona Isaya kuwa, Kila bonde litainulia, na kila mlima na kilima kitashushwa; palipopotoka patakuwa pamenyoka, na palipoparuza patasawazishwa! Is. 40:3-5; Luka 3:4-6. Katika kifo chake msalabani, aliandaa mahali kwa ajili yetu ili alipo nasi tuwepo. Yoh. 14:2,3,20. "Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu." Kol. 1:21,22; 3:3; 2Kor. 5:19. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake!"

Paulo anaelezea shukurani za kutokufungwa kwake na Mungu kwa ajili ya waamini wa Korintho kila anapofikiria utimilifu wa umoja wa imani yao katika Kristo. Anawaona wakiwa katika wema na neema, wenye uwezo wa kuishirikisha kwa moyo, ili kuleta mguso kwa wengine. 1Kor. 1:4,5. *"Mmepewa maarifa kamili na maelezo kamili kwa sababu ndani yenu ushuhuda wa kweli ya Kristo umepata uthibitisho." (New English Bible, Mst.6)* Tafsiri ya King James inasema, "Kama vile ushuhuda wa Kristo ulivyothibitika ndani yenu." Paulo anawatia moyo kukumbatia kwa ujasiri taraja la ufunuo kamili wa Kristo ndani yao. Sasa mwamini anaweza kujua bila mashaka kuwa kila anachohitaji tayari ni sehemu ya furushi la kipawa cha neema. Ushuhuda wa Kristo uliothibitika ndani yako hautakuacha uhangaike huku na huku, una uwezo wa kukusimamisha bila hatia mbele zake mpaka mwisho.Yesu ni uhakika wa kuachiliwa kwako, uzima na ushuhuda wake ni stakabadhi na hati ya uthibitisho dhidi ya mashitaka yote na shuku mbaya. *Biblia ya Amplified inasema, "Yeye ndiye uhakika wa uthibitisho wenu; yeye ni mdhamini wenu dhidi ya mashitaka yote."* Kufuatana na hili, Paulo anawasihi waamini wawe na nia moja





wao kwa wao; anamwonya kila mmoja wetu kunena lugha moja, (maana yake kunena mamoja) kwa sababu tunashiriki utukufu na hukumu iliyo sawa. 1Kor. 1:4-

13. Mtazamo wa Mungu ndio nuru pekee ya kutembea ndani yake. Matengano hayawezi kuvumilika! "Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote." Rum. 12:28. "Maana kwako wewe iko chemchemi ya uzima, katika nuru yako tutaona nuru." Zab. 36:9. Kufuatana na kazi ya Mungu ya neema katika kumtambulisha na kumwunganisha kila mtu katika Kristo, hapo haibaki nafasi ya wazo lingine lolote. Hakuna msisitizo maalumu wa mafundisho au mtindo binafsi wowote kutoka kwa mtu yeyote, awe ni Paulo au Petro au Apolo unaoweza kuharibu kiini kikuu cha Injili yake ya neema. Hatujaitwa kujulikana kwa ujuzi wa aina yoyote, mafundisho au tafsiri katika matumizi ya ukweli kama ulivyo katika Kristo. Ef. 4:21. Chemchemi huhifadhi na kulinda asili, wazo la Mungu lisilopunguzwa; Yeye ni Neno litokalo katika kinywa cha Mungu; yeye ni asili yetu na chimbuko zote za furaha ziko ndani yake!

Michanganyiko mitano ifuatayo ni thamani za urafiki wa maana ambao hauwezi kujichanganya kamwe:

- Upendo usio na masharti unafanya wepesi. (Kuthamini, kupenda).
- Uadilifu huleta tumaini.
- Kutokuwa na hatia; msamaha uliojengwa juu ya kuachiliwa kabisa; bilashuku, lawama au hatia.
- Umoja wa nia.
- Muda mrefu, taarifa zinazoendelea. (Kuishi kwa furaha baada yake).

1. Ufunuo wa ubunifu wa Mungu unautofautisha ukristo kutoka dini nyingine yoyote. Hakuna mganga wa jadi katika Africa alijipatia fedha zozote , isipokuwa wahanga daima walionyesha kutokufurahi au kukasirika! Imani ya ukristo wa kweli, sio kuhusu mtu kujaribu kujipatia upendeleo wa Uungu, au kujaribu kuhimiza tabia ya mungu mwenye hasira; hapa Mungu anaupatanisha ulimwengu wote na nafsi yake!

Rum. 5:10. Sio kuhusu sadaka anazozileta mtu; Sio mtu mwenye mwana-kondoo bora; Injili inafunua uanzilishi wa Mungu: "Tazama mwana-kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu!" Mwanzo 22:13,14; Isaya 53:7; Yohana 1:29. "Tunampenda kwa sababu alitupenda kwanza." 1Yoh. 4:19. Alitupenda tulipokuwa tungali tumeshikwa na dhambi. Rum. 5:8. Ikiwa dhambi iliweza kumtenga mwanadamu kutoka katika upendo wa Mungu, ndipo ukombozi ulikuwa hauwezekani. Yesu Kristo ndiye kipimo cha thamani ambayo Mungu anaiweka juu ya kila mtu. "Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo." Ef. 4:7. Aliikomboa sura yake na mfano wake ndani yetu. Luka 15:8,9. "Tulinunuliwa kwa thamani." 1Pet. 1:18,19. "Je mtu ni kitu gani , hata ukamtukuza, na kumtia moyoni mwako?" Ay. 7:17. "Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na mwanadamu hata umwangalie?" Zab. 8:4. "Mungu, fikira zako zina thamani nyingi kwangu; Jinsi ilivyo kubwa jumla yake; kama ningezihesabu ni nyingi kuliko mchanga; niamkapo nikali pamoja nawe!" Zab. 139:17,18. Mungu anaona matunda ya kazi ya upendo wake, naye husherehekea juu ya wazo la ukombozi na urejesho wetu kwake. Is. 53:4,5,11. "Atakushangilia kwa furaha kuu; Atatulia katika upendo wake. Atakufurahia kwa kuimba!" Sefania 3:17. Upendo unaiweka imani katika utendaji. Wagalatia 5:6.

2. Bila mashindano. Mungu mwenyewe anahakikisha uadilifu wa mwungano wake; "Kama sisi hatuamini, yeye hudumu wa kuaminiwa, kwa maana hawezi kujikana mwenyewe."





2Tim. 2:13. "Ni nini, basi, ikiwa baadhi yao hawakuamini? Hasha! Mungu aonekane kuwa amini na kila mtu mwongo!" Rum. 3:3,4. Anatamani kutuweka mbali na mashindano yote kuhusu uadilifu ulio wazi, wa kusudi lake la milele; (katika mambo yetu ya kibinadamu tuliweza kuapa kiapo kwa mamlaka ya juu, ili kuongeza uzito kwa makusudio yetu). Mungu anatumia mtindo ule ule ili kutuvuta kwenye hukumu yake isiyobadilika, na kutenda mambo kana kwamba Neno lake haliwezi kutumainiwa. Kwa hiyo anaapa mwenyewe, kukiwa hakuna mamlaka iliyo kuu kuliko kiti chake cha enzi, kwa maana Mungu ni mpatanishi wa hakika kwa neno lake. Ebr. 6:9-20. Ukombozi wa mwanadamu haupo katika uwiano wala haupo katika hatari! Yesu ni 'ndiyo' ya Mungu ya milele kwa mtu; katika ubinadamu wake, alifanyika kuwa hakika na utimilifu wa kila ahadi aliyokuwa nayo Mungu katika nia yake kwa wanadamu! 2Kor. 1:18-22. "Mungu hawezi kusema uongo." Tit. 1:2,3. "Ni neno la kuaminiwa. Kwa maana kama tukifa pamoja naye, tutaishi pamoja naye pia." *"Ibrahimu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu (Gr. doxa, shauri) huku akijua hakika ya kuwa Munguaweza kufanya yale aliyoahidi. Kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa ni haki." Rum. 4:20-22. Tafsiri ya Knox*. "Neno ni kweli hakika na thamani kwa taraja letu lisilobadilika." 1Tim. 4:9. "Kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe wa Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini!" 1Thes.2:13. *Tafsiri ya Ujumbe.* Yesu ni hakika ya mwanzo na mwisho wa imani yetu. Ebr. 12:2. Imani ya Mungu ndiyo chemchemi ya imani yetu." Rum. 1:16,17. Mwanadamuni wa asili ya imani; "Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, 'Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena' sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena." 2Kor. 4:13. Mtiririko wa maelezo haya ni wa kanuni ya kioo:2Kor. 3:18; 4:1-

18. "Kwa kuwa tuna huduma hii, kwa jinsi tulivyopata rehema, hatulegei." Hakuna upinzani ulio na jambo la kushawishi kwa namna yoyote. Mamboyaliyomo na mchanganyiko mkuu wa imani yetu, ni kuakisi katika kioo kwa mwanadamu katika sura ya Kristo, ambaye ni mfano wa Mungu. Kufuatana na uadilifu wa Mungu, Biblia inafanyika kuwa hati ya uthibitisho kamili wa kuanzisha jukwaa halali na uhakika wa utambulisho wa kweli wa mwanadamu na kuachiliwa kwake. Maandishi na sura ya Kaisari yanakitofautisha kipande cha bati kuwa toleo halali. Kwa njia iyo hiyo, Injili inafunua maandishi na mfano wa Mungu katika suraya Kristo kama toleo halali kumkomboa mwanadamu.

3. Bila hatia. Dhamiri ya dhambi itabatilisha matokeo ya msalaba, na kuharibu kila msingi wa uhusiano wa maana. Uhusiano uliojengwa juu ya hatia, shuku mbaya, auhukumu, hauna mwendelezo wa baadaye. Ili urafiki kuwa wa thamani na kutokuwana hatia, si jambo la mjadala. Hali ya bila hatia aliyotembea nayo Adamu kabla ya anguko, ni hali ile ile ya bila hatia ambayo Kristo hufurahia katika mwungano na Baba yake; na sasa ni fursa iliyorejeshwa kwa kila mtu. Kila shitaka dhidi ya mtu imefutwa; mtu anasimama akiwa amethibitika kwa kuachiliwa kikamilifu. Mwana mpotevu hayuko kaika kujaribiwa; anasimama akiwa amehesabiwa haki kana kwamba hajawahi kutenda dhambi! "Kristo alikufa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki." "Basi tukisha kuhesabiwa haki itokayo katikaimani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo; ambayekwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo tunasimama ndaniyake." Rum. 4:25; 5:1,2. Kazi ya Mungu katika Kristo kwa niaba ya wanadamu imetenda kazi kubwa zaidi kuliko kuleta msamaha wa dhambi tu. Amevunja utawala wa dhambi katika maisha yetu! Rum. 8:1-5. "Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na





kutokutahiriwa kwa mwili wenu, (kutokutahiriwa kwa mwili, katika Griki, ni maisha yaliyotawaliwa na via vya uzazi). Aliwafanya hai pamoja naye, akisha kutusamehe makosa yote; akisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani; akisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo!" Kol. 2:13-15. Tafsiri ya kingereza ya 'Contemporary' inasema, 'Mungu aliutumia mwili wa Kristo ili kuihukumu dhambi.' Sifa ya dhambi ya kuutawala mwili wa mwanadamu, imepingwa na kushindwa milele katika mwili wa Kristo. Tafsiri ya Knox inasema, Ametia sahihi kuhusu usalama juu ya kifo katika asili yetu." Rum. 8:3. Injili inafunua kuwa imani inatushirikisha dhamiri ya haki badala ya dhamiri ya dhambi. Ebr. 9:9-14; 10:1- 4,14,22. Kifo kinaleta mwisho wa dhambi, kwa kuwa Kristo aliteswa kwa ajili yetu katika mwili, (alikufa kifo chetu; mlikuwa katika nia yake yote), akifikiria maana yakukujumlisha katika yeye. Kwa hiyo jitie nguvu nia zenu na kusimama imara dhidi ya shambulio lolote. Kwa ujasiri mweze kuishi wakati wenu uliobaki katika mwili, yaliyovuviwa na kusudi la Mungu, pasipo kuwa na tamaa za kibinadamu zilizopotoka." 1Pet. 3:18; 4:1,2. Kifo alichokufa, aliifia dhambi, mara moja kwa wote; bali uzima anaoishi, anamwishia Mungu. Kwa hiyo na wewe ni lazima ujihesabu kuwa umekufa kwa dhambi, na umekuwa hai kwa Mungu katika ushirika pamoja na Kristo Yesu. *(Gr. logitzomai,* hatima ya hoja*)*, "Kwa tendo moja la haki, watu wote walihesabiwa haki yenye uzima." Rum. 5:18. Tafsiri ya 'Phillips.' Kila shitaka dhidi ya mwanadamu imefutwa kwa mafanikio. Yoh.12:31,32; Uf. 12:9-12;Zab. 103:2,3,10-12; Zek. 3:1-9.

4. Umoja wa nia sio jambo la uchaguzi wa hiari; ni utimilifu wa imani yetu. Umoja huu unaleta urafiki badala ya ugomvi. Paulo anaona kuwa umoja katika Kristo unaleta ulinganifu mzuri wa

mwenendo kwa kusema, "Basi ndugu, nawasihi kwa jinala Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja." 1Kor. 1:10. "Twaamini, na kwa hiyo twanena." 2Kor.4:13. "Ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu, katika Kristo. Filem. 6. "Nina matumaini kwenu katika Bwana, ya kwamba hamtakuwa na nia nyingine." Gal. 5:10. Injili yote inafunua kushirikishwa kwetu katika Kristo. Si ajabu kwamba Pauloanasema kwetu, kushindana sisi kwa sisi au kujilinganisha sisi kwa sisi, ni kutokuwana akili. 2Kor.10:12.

Hili linahitimisha kwamba hakuna tofauti binafsi, matakwa binafsi au upendeleo usiona sababu utakaovumilika juu ya kweli ya ajabu ya kazi ya Mungu ya neema na upatanisho. Paulo anamkumbusha Tito, "Wasimtukane mtu yeyote, wasiwe wagomvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote. Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukiana. Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili kwa kufanywa upya na Roho Mtakatifu." Tito 3:2-5. "Msimlipe mtu uovu kwa uovu; angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote. *(Gr. pronoeo,* maana yake; tazamia, fikiria au kujua kabla; *kalon,* uzuri, kitu kilicho na thamani kubwa.) Mmekuwa na zaidi ya uwezo, ndani yenu kuna kila namna ya kuwafanya mwe na amani na kila mtu, bila kujali wanawatendeaje! Usijisumbue hata kama unahisi kutendewa. Hapa kuna mkakati mzuri: uyaangalie mahitaji ya adui zako na wote wanaokuchukia; walishe wanapokuwa na njaa, na uwanyweshe wanapokuwa na kiu!" Rum. 12:17-





20. Hapa Paulo amenukuu kutoka Mithali 25:21,22. "Kumpalia makaa ya moto kichwani pake" kunafananishwa na mfuaji anavyoyeyusha chuma katika kalibu, si kwa kuweka tu juu ya moto, bali kwa kuweka makaa ya moto juu yake, hivyo kuzidisha joto na mchakato wa haraka! Kwa hiyo, haya matendo ya wema, yataondoa taka-taka katika akili za adui yako, na kumpata kuwa rafiki yako! Munguanaona dhahabu katika kila uhusiano. Alitupata tulipokuwa tungali mbali naye! Rum.5:8,10. "Wema wa Mungu ulikuchochea kwa nguvu ya ushawishi kukuingiza katikabadiliko kamili la nia." Rum.2:4. "Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, bali walikufa wote. Hata imekuwa, sisi tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili." 2Kor. 5:14,16. Jifunze na kukariri maandiko yafuatayo kwa uangalifu mkubwa: 1Kor.1:30;2:2,7,8; Mdo 10:15,28; 1Yoh.1:7; 5:9,10,20; 2:8-10; Zab.36:9; 2Kor.1:18- 20; Filem.6: Ef.4:7; Yak.3:9; Ebr:2:11. Kwa kuwa Mungu hajichanganyi kuhusiana nasi,tunaweza kufanikiwa kuwa na umoja katika nia na kuungana katika wazo moja.

5. Kuishi kwa furaha baada ya hayo! Hiki sio kikaango ndani ya chungu, kitu kinachochoma na kukimbia! Injili hii inaupima umoja kuwa ni wa kuufurahia bila kizuizi, usio na mipaka, usioingiliwa na mambo mengine baadaye! Kwa Ayubu, wazo hili lilikuwa jema sana na la kweli. Hofu ilitawala uhusiano wake na Mungu. Ay.1:5; 3:25. Alipoangalia maisha yake aliongelea kuhusu siku za "hali ya urafiki wake na Mungu." Ay.29:2-4. (RSV). Hili linatuonyesha kuwa aliishi chini ya hofu iliyoendeleakiasi kwamba kipindi cha baridi kilikatisha furaha ya urafiki huu! Mungu hana jambokubwa zaidi kuliko nyakati za baraka katika nia yake. Ef.1:4,5. Inafunua kuwa sisi nindoto ya upendo wa Mungu wa milele. Katika Kristo, pumziko la sabato sio siku tena, bali ni sherehe ya ukombozi kamili; ni mahali pa Mungu pa furaha isiyozuilikaya mwanadamu, na mahali

pa mwanadamu pa furaha isiyozuilika ya Mungu. Mtume Yohana, rafiki wa karibu wa Yesu aliandika, (miaka 60 baada ya Yesu kujitenga nao katika mwili,) ushirika usiokatishwa, ambao si kwamba aliendelea kufurahia tu, bali anatamani kila mwamini aushiriki kikamilifu ndani yake. "Ujumbe wetu unahusu lileNeno, ambalo ni uzima; lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia kuhusu yeye, tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa. Ndiyo, ni uzima ambao umepambazuka, na sisi tu mashahidi wa kuona kwa macho. Ninawaandikia haya ili furaha yenu iwe timilifu." (Tafsiri ya Knox.) Mungu ni nuru, na ndani yake hana giza kabisa. "Kutembea katika nuru kama yeye alivyo katika nuru, kunatushauri kujiona katika Mungu kwa jinsi ya mwili. Sasa, kuungama dhambi kunaleta maana mpya kabisa. Neno la Kigriki lililotafsiriwa kwa maana ya kuungama, limetokana na maneno mawili; *homo + logeo,* likiwa na maana ya kusema jambo lile lile. Kwa hiyo badala ya kumwambia Mungu habari nyingi kuhusu dhambi zako, unaiambia dhambi habari nyingi kuhusu ukombozi wako. Mungu hahitaji taarifa, bali nguvu za giza zinafanya hivyo! Huwezi kufanikiwa kujidanganya mwenyewe kwa kuishi maisha yenye njia mbili, ukiigiza 'jambo la ushirika' huku ukiendelea kuificha dhambi katika maisha yako! Ihubirie dhambi katika mamlaka sawasawa na utoaji wa Mungu katika Kristo; damu yake inatusafisha dhambi zote. Yohana aliwaandikia waamini kufuatana na viwango tofauti vya ukuaji wao; watoto wadogo, vijana na akina baba. 1Yoh.2:12-14. Kwa watoto wadogo alisema, "Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi, (dhambi si kitu cha kawaida) tunaye mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki; naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali nakwa dhambi za ulimwengu wote." Hakuna mwenye sifa ya kukuwakilisha kuliko yeye! 1Yoh. 1-2:1,2. Pia jifunze na kukariri maandiko





yafuatayo: Ebr.9:12; Kol.2:13-16; Rum.6:1,6,7,11,12,17; 8:1-4; 1Pet.4:1,2; Kol.3:1-3.

## MAFANIKIO YA MSALABA

Injili inafunua jinsi Mungu alivyofanikiwa kufuta matokeo ya anguko la Adamu. Ili Injili iwe habari njema, ni lazima, angalau ishirikishe ukombozi ambao unamrejesha mtu kwenye ndoto ya upendo wa asili wa Mungu. Katika Efeso 1:4 Paulo anamwona mwanadamu akiwa ameshirikishwa katika Kristo tangu kabla ya kuwekwa msingi wadunia; kwa sababu ya ushirika huu, kila kitu kinachotokea ndani au kupitia Kristo kinamjumlisha mtu na nafsi yake. "Kwa Mungu mmepata kuwa katika Kristo" ndivyoasemavyo Paulo katika 1Kor.1:30. Umoja huu sio matokeo ya kudhania tu kwa mtu au fikira za mema, "Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake!" 2Kor.5:18,19.

Kuna jambo kubwa sana na matokeo makubwa yaliyotokea kwa mwanadamu katika Kristo, kuliko lolote ambalo lingeweza kusemwa dhidi ya mwanadamu kama matokeo ya anguko la Adamu. Kumbukumbu ya historia yote haiwezi kuleta ushahidi wa kutosha dhidi ya mwanadamu kuvuruga au kufuta maamuzi ya Mungu ya kumwachilia! Kipawa cha Mungu cha bure kisichopimika kinaondoa makosa katika matokeo haya. "Kwa maana ikiwa kwa kukosa kwake yule mmoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mungu, na kipawa kilicho katika neema yake, mwanadamu mmoja Yesu Kristo, kimezidi kwa ajili ya wale wengi. Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki walihesabiwa haki yenye uzima." Rum.5:15,18. (Tafsiri ya Weymouth). "Tendo moja la Adamu na tendo moja la Kristo yako sawa, katika hayo yote, mwanadamu aliguswa nayo, ingawa matokeo yake ni tofauti kabisa. Rum.5:18. (Tafsiri ya Johnson). Hali ile ile ya ubinadamu iliyoangukia chini ya





laana ya dhambi ya Adamu, sasa inahubiriwa katika Injili ya Yesu Kristo! Mungu aliyoyakamilisha katikaKristo, ni tofauti na malinganisho ya kiasi cha matokeo ya dhambi ya Adamu.

J.B.Phillips anaandika (1955) katika dibaji ya tafsiri ya kitabu cha Matendo ya mitume yafuatayo: "Hivi sasa katika uinjilisti wa siku hizi, mbao za jukwaa ndiyo msisitizo tena na tena juu ya hali ya dhambi ya mtu. "Biblia inasema, 'Wote wametenda dhambi,' mwinjilisti wa siku hizi atapiga kelele, "Bible inasema, 'Hakunamwenye haki hata mmoja.' Biblia inasema, 'Haki yetu yote ni kama mavazi machafu." Lakini Luka akiandika kitabu cha Matendo, alionyesha kuwa hajui lolote kuhusu msisitizo huu. Badala yake aliandika juu ya ujuzi wa Petro na Korinelio' Mungu alipomwonya kutokumwita mtu yeyote najisi au mchafu! Kwa kweli, mtindo wa siku hizi wa kuamsha hatia, kwa kunukuu vifungu vya maandiko yenye kutenga watu, hayapatikani kabisa katika kitabu cha Matendo."

Mafanikio ya msalaba na mguso mpya kwa maana ya ufufuo, yalikuwa ushuhuda katika kitabu cha Matendo ya waamini wa kwanza. "Roho Mtakatifu alilithibitisha Neno la neema yake kwa ishara na maajabu zilizofuatana na mahubiri yao; na nenolikaenea, na hesbu ya wanafunzi ilizidi sana!" Mdo 6:7; 14:3.

Injili inatangaza kutokuwa na hatia kwa mwanadamu; ndiyo stakabadhi inayothibitisha kuachiliwa kwa mtu. Katika shughuli yoyote stakabadhi inawakilisha maelezo na rejea halali ya malipo sahihi; ni utambulisho wa kuandikwa kwa malipohayo. Sasa badala ya mwanadamu, kuikabili hukumu inayomstahili, kuna uamuzi wamwisho, Msamaha wa dhambi na upendeleo. Msingi halali kuhusu uamuzi huu, unaelezwa katika mahubiri na mafundisho ya Injili ya neema. Dhana ya kuachiliwa kwa mtu ina maana kuwa, namna zote za kuleta

mashitaka, hukumu na laumu vimeondolewa; mwanadamu ametangaziwa kuwa hana hatia, na kwa kawaidaameachiliwa kutokana na deni! "Tumefanyika kuwa hai katika ufufuo wake; hili linathibitisha kuwa makosa yamesamehewa. Mwili wa Kristo ulitundikwa msalabani,uliwakilisha kufutwa kwa hati iliyoandikwa ya hatia ya mwanadamu. Mshitaki wa mwanadamu sasa anasimama akiwa ameanikwa peupe, akiwa uchi na mashaka, na silaha zake zikiwa zimenyang'anywa kwake, mawindo yake yameokoka kutokana na udhalimu wake!" Kol.2:13,14. Shetani hawezi tena kutoa rushwa kwa hatia ya mtu.Mungu amefanya vya kutosha kumhesabia haki mwanadamu; ufufuo wake kutoka kwa wafu unatangaza kuhesabiwa haki yetu kwa ushindi. Rum.4:25.

Ufunuo wa haki ya Mungu ndiyo siri ya nguvu ya Injili. Rum.1:16,17. "Kutoka imanihata imani" maana yake Mungu anaamini yanayofunuliwa na Injili, na tunaichukua imani kutoka katika ufunuo huo; Injili inatangaza kwa njia tofauti namna Mungu anavyosema kuhusu mtu; anayoyatangaza kuwa ni kweli ya mtu huyo katika Kristo.1Kor.1:30.

Katika vipeperushi vingi vya Injili kwa miaka mingi, vilitangaza Rum.3:23. katika hali ya mtiririko wa kuwatenga watu, wakati mistari 21,22, na 24-26 inafunua ushindi wa msalaba! Watu wale wale waliosimama wakiwa wamehukumiwa, sasa wanasimama wakiwa wamehesabiwa haki katika Kristo! Jinsi Mungu anavyotafsiri kifo na ufufuo wa Yesu, kunatupa ufafanuzi wa mwisho na mguso wa Injili. Sasa anatamani kuvuta macho yetu ili kuona yale anayoyaona katika matunda yauchungu wa nafsi yake. Is.53:11. Mkazo wa Yohana 10:10, sio tu kwamba mwivi anakuja kuiba, kuua na kuharibu, bali kwamba Yesu alikuja ili tuwe na uzima tele! "Maana kwako wewe iko chemchemi ya uzima, katika nuru yako tutaona nuru. Zab. 36:9. Ushuhuda wa Mungu ndio





madai yetu pekee ya utukufu. Yoh. 5:9-11,20. "Hata imekuwa, tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili!" 2Kor.5:16. "Mungu amenionya nisimwite mtu awaye yote kuwa najisi au mchafu." Mdo 10:28. Hakuna shauku binafsi, sifa, uzao wa kiungwana au mafanikio yanayoweza kumpa mtu tofauti zaidi au kutambulika kwa mtu, kuliko ukweli wa kutambuliwa na kujumlishwa katika Kristo! Filipi 3:4-9. Paulo anailinda kwa bidii na wivu Injili hii. Gal.1:6,7,11,12, Gal.2:5. "Injili yangu ni kumhubiri Yesu Kristo, sawasawa na ufunuo wa siri (kujumlishwa kila mtu ndani yake, 1Kor. 2:6-8; Hos.6:2.) iliyositirikatangu zamani za milele, ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote." Rum. 16:25-27. Watawala wa giza walishindwa kuelewa kuwa wanadamu wote waliwakilishwa katika kifo na ufufuo wa Kristo; kile walichoshindwa kukiona kilileta madai ya nguvu juu ya mwanadamu hata kufikia sifuri. Neno la Kigriki, *katargeo, lina maana ya* kutolewa bila maana kabisa!1Kor.2:6. Mungu alifikisha na kuagiza lililotokea katika Kristo kuwa ni urejesho wamwanadamu kwa shauri la asili (utukufu) wa Mungu. Adui hawezi kufanya lolote pasipo kibali cha mtu; uwezekano wa nguvu pekee ambazo adui aliyeshindwa anaweza kufikiria, ni kutumia kutokuamini kwa mtu na ujinga wake, ili kumshswishimtu ajidanganye mwenyewe na kusahau yeye ni mtu wa namna gani! Yak.1:8,18,22-25. Yesu alisema kuwa ili kuendelea katika Neno lake, ni lazima kuijua kweli, na kuujua ukweli wa uwana ndio uhuru wa kweli. Yoh.8:31,32,35,36. Kwa kawaida kweli huzaa imani; imani inahuishwa katika kusikia kwetu; hili ni la kutazamiwa kwa moyo kufurika, na ushawishi wa uadilifu wa mpango wa Mungu kama ulivyofunuliwa katika Kristo. Rum.10:17; Ef.1:13; 4:21. Kusudi la Mungu la milele daima limekuwa kwa ajili ya mwanadamu kushiriki katika utukufu wake; imani huona ushindi wa msalaba katika maana yake kamili. 1Pet.1:10-13.

Ukombozihupata msisitizo wake na ufafanuzi katika ukweli wa kwamba, mwanadamu aliumbwa kwa sura na mfano wa Mungu; kuakisi kwa kweli kwa muumbaji wetu kunangojewa kuamshwa ndani yetu kwa njia ya Injili ya imani. Mw.1:26,31. Injili huthibitisha pasipo mabishano kuwa Mungu aliikomboa sura na mfano wake ndani ya mwanadamu.

Historia iliandika kifo na ufufuo wa mtu mmoja; milele inaandika kifo na ufufuo wa kizazi cha Adamu! Mungu anaona katika kifo cha Yesu, kifo cha kila mtu. 2Kor.5:14;1Kor.15:22.

Kujumlishwa kwa mwanadamu katika Kristo ndio utimilifu wa neema. Manabii waliliona: "Ni nani aliyesikia neno kama hili? Ni nani aliyeona mambo kama haya? Je, nchi yaweza kuzaliwa siku moja? Taifa laweza kuzaliwa mara?" Is.66:8. "Baada ya siku mbili atatufufua; siku ya tatu atatuinua, nasi tutaishi mbele zake." Hos.6:1,2,7. Kuunganishwa kwetu katika kifo na ufufuo wa Yesu, kulitabiriwa miaka 800 K.K. kupitia nabii Hosea, na miaka 700 K.K. kupitia nabii Isaya. "Na mkono waBwana amefunuliwa nani?" Is. 52:10; 53:1,4,11. Petro aliona haya: "Mungu amenionyesha kuwa nisimwite mtu yeyote najisi au mchafu." Mdo 10:28. Petro alitambua kuwa kuna jambo lilitokea kwa mwanadamu katika kifo cha Yesu. Tulizaliwa upya katika ufufuo wake! 1Pet.1:3. Luka aliandika: "Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa, ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama Daudi alivyotabiri katika Zaburi ya pili, ''wewe ndiwe mwanangu, mimi leo nimekuzaa.' Mdo 13:30-33.Ufufuo wa Yesu unatangaza uzao mpya wa mwanadamu.

Paulo aliona haya: "Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo." Ef.2:5. "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; yaaninimeunganishwa naye katika kifo kana kwamba ni kifo chake." Gal. 2:20; Rum.6:5;





Kol.2:11-13; 3:1-4; Gal.3:26; 4:7; 2Kor.5:16-19. Yohana aliona haya: "Nasi twajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, yaani, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo. Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele." 1Yoh.5:20. "Neno lililo kweli ndani yake ndivyo lilivyo ndani yenu." 1Yoh.2:7,8. Yesu aliona haya: "Naye Yesu akawajibu, akasema, saa imefika atukuzwe Mwana wa Adamu; Amin, amin, nawaambia, Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; baliikifa, hutoa mazao mengi." Yoh.12:23,24. Sasa tunaona haya: Paulo anatuombea kwamba macho ya ufahamu wetu yafumbuliwe, ili kwamba tuijue siri ya kusudi lake.Ef. 1:9,10,17-19; 2:1-10. "Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake." Rum.6:5,6. "Nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi." Rum.6:11. (Tafsiri ya Knox. Neno la Kigriki, *logizomai*, maana yake, mwisho wenye mantiki; huu ndio ukamilifu wa imani, inayotushauri kuwa, si mawazo ya kutaka au kutangulia kufikiri mwenyewe namna hii! Kwa kweli, hakuna njia nyingine ya kujiona mwenyewe pasipo kudanganya au kuipindua kweli! Sheria ilipotakiwa kuwajibika kwa utii na matakwa,Injili ya neema yake inatutaka tuwe na hitaji la imani. Hii inafungua namna nyingine ya utii; Utii wa imani. Rum.1:5,16,17; 16:25,26. Sheria ilifunua jinsi mwanadamu alivyofanyika kuwa mwenye dhambi sana, wakati Injili inafunua jinsi mwanadamu alivyofanyika mwenye haki sana. Rum.7:13. Mwisho wa dunia utaona haya! "Bwana ameweka wazi mkono wake mtakatifu machoni pa mataifa yote; na ncha zote za dunia, zitauona wokovu wa Mungu wetu." Is.52:10. Habakuki,(ambaye jina lake lina maana ya kukumbatia), ni nabii aliyeiona haki kwa imani, 2:4. Katika sura ya 2:2 anasema, "Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji."

Tafsiri ya kingereza ya Die Contemporary inasema, "Ndipo Bwana aliniambia, 'Nitakupa ujumbe wangu katika namna ya maono. Uandike kwa wazi vya kutosha ili iweze kusomwa kwa mng'ao." Na ndipo katika msitari wa 14 anatoa usemi maalumu, "Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari." Zaburi 98:1-3 inaandika wimbo ufuatao: "Mwimbieni Bwana wimbo mpya, kwa maana ametenda mambo ya ajabu. Mkono wa kuume wake mwenyewe, mkono wake mtakatifu umemtendea wokovu. Bwana ameufunua wokovu wake, machoni pa mataifa ameidhihirisha haki yake. Miisho yote ya dunia imeuona wokovu wa Mungu wetu." Falme zote na mamlaka zitaona haya: "Kupitia Ekklesia, (wote wasikiao na kuitikia sauti ya asili yao ya kweli na utambulisho), hekima mbalimbali ya Mungu iweze sasa kujulikana kwa falme na mamlaka. Na kwa wakati ujao, ataendelea kufunua ndani yetu , utajiri usio na kiasi wa neema yake, kuonyesha wema kwetu katika Kristo Yesu." Ef.2:6,7; 3:10.

Paulo anaiona huduma yake na utume kuwa ni tunda la neema, ambalo sasa linamhimiza kuuleta utii wa imani. Rum.1:5. Neno la Kigriki la utii ni, *hupakouo, (upo,* kujitoa chini ya *+akouo,* kusikiliza kwa ajili ya), kusikia na kutofautisha kwa ufahamu sahihi. Paulo anatamani kuwafanya watu wote wasikie. Ef.3:9. Yakobo anaona siri ya kioo, mahali utambulisho wetu wa kweli unapofunuliwa, kama sheriakamilifu ya uhuru. (Sheria ya moyo wa hiari) Yak.1:23-25. Matendo yetu hufanyikakwa kuona kwetu ukweli kuhusu sisi wenyewe. Hakuna tena matendo kuwa ni kitu,au kutenda ili kujikamilisha wenyewe, bali kufanya kwa sababu imani yetu inajua kuwa sisi ni nani! Ukiwa umejua kuhusu utambulisho wako wa kweli mbele ya upinzani, hiyo ndiyo siri ya maisha ya utimilifu. Yak.1:2-4,17,18. Injili inabakia katika nafasi ya kwanza ya kile nionacho, wala si kile nifanyacho; hata kufa kwangusi kutenda, bali ni kuona;





daima kuona kunaleta kutenda. Sheria ya imani inafunuajinsi utii wa Kristo ulivyofuta matokeo ya kutokutii kwa Adamu. Rum.5:19. Maana ya haraka ya utii wa Kristo inatufungulia mamlaka, ambayo kwa hayo tutawezakuharibu kila ngome, na kuteka kila fikira inayotufanya watumwa wa mawazo duni au kutojitambua. (Tazama 2Kor.10:3-5, ambapo tafsiri ya Biblia ya King James, inatafsiri sahihi, "Utii wa Kristo" badala ya 'utii kwa Kristo' kama na tafsiri nyingine nyingi zinavyosema kimakosa. Hii inafanya tofauti mbaya na kubwa mno. Kumtii Kristo kunamfanya mtu adumu katika kuwekewa mipaka ile ile na mifadhaiko aliyoizoea chini ya sheria; kutokuendelea na kutokuweza kwake kunaleta hisia za hatia na kushindwa kusikoepukika, wakati utii wa Kristo unamuunganisha mwanadamu katika mafanikio yasiyo na mipaka ya ufanisi wa Kristo, aliotenda kwaniaba yetu. Hakuna upinzani kwa ajili ya maana ya utii wake unaoweza kuvumilika.Muda wa imani ni sawa na matokeo ya nuru inavyoondoa giza, bila kutumia nguvu.Giza halifuti kweli , ila inajificha kutoka katika mwonekano ambao upo tayari, ambaonuru inaufunua.

Bado kuna uwezekano kwa mtu kupuuza au kudharau kweli ya wokovu na kufanya sehemu ndogo sana, lakini haiwezekani kufanya sehemu kubwa sana kwa wokovu mkuu namna hii.

Ukombozi unaweza kuwa chini ya makisio, lakini hauwezi kutiwa chumvi nyingi mno.Ebr.2:3; 2nyak.9:5,6; Luka 11:31. Gundua kiasi cha upendo wa Mungu usiopimika unaopita ufahamu. Ef.3:18-20. "Waamini wote wawili wanaweza kutambua kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zao, na kufurahia katika msamaha wake; lakini mmoja wao, badala yake anaona kwa kina zaidi na kuelewa kuwa, pia Kristo alikufakwa ajili ya hali yetu ya dhambi." (George Peck 1880). "Je inawezekana kuwa sasa tuna kibali cha kutenda dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? La hasha! Hatuwezi kuwa wafu

na tuwe hai kwa dhambi kwa wakati mmoja.” Rum.6:1,2. “Kusulubiwa kwetu pamoja na Kristo, kuna maana kwamba, dhambi imepoteza haki yake ya kutumia miili yetu kama gari lake. Mtu mfu hadhuriki na nguvu ya dhambi. Kwa kuwa tumejumlishwa katika kifo cha Kristo kwa imani, ndio msingi ambao juu yake sisi nasi tunashiriki katika uzima wake.” Rum.6:6,7. “Tumekwisha kupita kutoka dhambini kweli kweli, sawasawa na mfu alivyokwisha kupita kutoka uzimani.” Rum.6:6. (Tafsiri ya Way). “Sasa tunaweza kuhitimisha kwa ujasiri kuwa, hakika tumekufa kwa dhambi, na kuishi katika ushirika na Mungu kwa njia ya Kristo. Miili yetu ni mizuri kama vile mfu alivyo mbali na utawala wa dhambi.” Rum.6:11,12. “Juu ya msalaba, mwili wake mwenyewe ulichukua uzito wa dhambi zetu.” (Tafsiri ya Knox). Kwa hiyo tuliifia dhambi, na sasa tunaitwa hai kwa haki; kwa kupigwa kwake sisi tumepona! 1Pet.2:24; 4:1,2. “Katika Kristo Mungu alishughulikia dhambikwa njia ambayo alizihukumu nguvu zake katika milki iliyodaiwa kuwa ngome yake,yaani mwili wa mwanadamu!” Rum.8:3.





## YESU - UFUNUO WA UTAMBULISHO WA KWELI WA MTU

(Ushuhuda wa ukweli)

Asili ya mtu imepigwa chapa katika nia ya Mungu milele. Mw.1:26. “Kabla sijakuumbakatika tumbo nalikujua.” Yer.1:5. Ushirikiano usiotenganika ulitokea tangu kabla ya kuwekwa msingi wa dunia, unaomtambulisha mtu katika Kristo. Ef.1:4. Katika Kristotunaona kielelezo na sura ya asili iliyokusudiwa ya maishayetu. Rum. 8:29.(Tafsiri yaThe message). Maneno mawili muhimu sana katika Biblia, ni haya: “katika Kristo” Ushirika huu ni ufunguo unaofungua siri ya Biblia; haiwezekani kuielewa Biblia au ukombozi katika nuru nyingine yoyote. Neno “shirikisha” lina maana kuwa, kunatokeaumoja kati ya sehemu mbalimbali unaofanya isiwezekane kudharau au kuitenga sehemu yoyote kutoka kwa nyingine, wakati nyingine imeletwa akilini. Katika nia ya Mungu,mara Yesu anamwakilisha mwanadamu; ushirika huu unafanya isiwezekane kwa Mungu kumweka mbali au kumtenga mtu kutokana na uzima, kifo, ufufuo na kutukuzwa kwaMwana wake. Mungu ana ufahamu wa ndani na mwanadamu katika hali halisi ya wazolake la milele. Katika upana wa kuwapo kwake, anamwona mtu katika sura yake na mfano wake mwenyewe. “Mungu alipotufikiria na kututengeneza katika umoja na Kristo,alikuwa na ubora wa maelezo akilini kwamba ungekuwa ni wa kudumu sawa na matazamio yake ya kweli kwa uumbaji wetu wa asili.” Ef.2:10. Neno la Kigriki, *hetoimatzo,* maana yake hasa, ni kutayarisha kabla ya wakati, limechukuliwa kutokautamaduni wa nchi za mashariki, wa kumtuma mtu mbele ya safari ya mfalme, ili kutengeneza njia na kuifanya ipitike. Katika Kristo, Mungu alifanya njia kuu ya kifalmekwa ajili yetu, kila kizuizi kimeondolewa ili tuweze

kutembea kama wafalme! Is.40:3,4.Katika mtiririko wa habari ya Waefeso 2, Paulo anafunua jinsi Mungu alivyoturejeshakatika utawala, mkono wake wa kuume kupitia umoja wetu na Kristo katika kifo naufufuo wake. Hivi sasa tumeketi pamoja naye na kushiriki ushindi wake na enzi juu yadhambi zote na mamlaka za giza. Historia haikuweza kuleta upinzani wa kutosha ili kubatilisha au kupunguza sura ya Mungu ndani ya mtu. Asili yetu inafunua mwanzo wa matokeo makubwa kuliko lolote ambalo upinzani ungeweza kukana; wakati, muda na historia vinaweza tu kuandika na kusajili nyakati na matukio yanayopita upesi; imani inafunua kweli katika roho na kipimo cha milele. Utajiri wa ushirika huu wa ndani unaumba msingi wa mapambano yetu ya kiroho. Haya ni mafuta ya ushawishi wa imani na maelezo ya mwisho wa uzima. Kufuatana na umoja huu, kuna siri na kweli ya Injili. Yesu haoni haya kumwita mtu ndugu yake, kwa kuwa wanashiriki asili moja. Ebr. 1:1-3 na 2:11.

Maana ya kujumlishwa kwa mwanadamu katika Kristo inaishia katika ufunuo wa kifochake kuwa ni kifo chetu pia, na ufufuo wake wa ushindi kuwa ni uzao wetu mpya. Yesu akiwa ndiye Adamu wa mwisho, anamaliza kizazi cha anguko la Adamu. 1Kor.15:45; 1Pet.1:3. Alipofufuliwa kwa nguvu za Mungu, namna mpya imezaliwa, mambo ya kale yamepita, tazama yote yamekuwa mapya! "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya." "ikiwa" sio sharti bali hitimisho! 2Kor.5:17. "Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" Rum.8:31. Habari Njema inafunua kuwa Mungu yuko kwa ajili yetu! Malaika walitangaza wema na kupendezwa katika mwanadamu, walipotangaza kifo cha Yesu. Hizi ni habari njema za furaha kuu, itakayowajia watu wote! Luka 2:10,14. "Kwa yeye mmepata kuwa katika Kristo." 1Kor.1:30.



KUKUMBATIA KIMUNGU

Ufunuo wa Kristo hauna maana bila kujumlishwa kwa mwanadamu ndani yake! "Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho." Ef.2:5,6; Hos.6:2. "Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli."Yak.1:18. Kusikia neno la kweli, ni kuona sura ya uzao wako wewe mwenyewe jinsiulivyo. Yak.1:22-25. Ukweli kuhusu mwanadamu umefunuliwa katika Kristo; hii ndiyo siri ya neema, Mungu alitudhihirisha katika Kristo! "Mmoja kufa kwa ajili ya wote, kunatufanya kubaki na jawabu moja tu kuwa, basi wote tulikufa!" 2Kor.5:14.Injili ni ukweli kuhusu sisi kama ilivyoandikwa katika Kristo. Ef.1:13; 4:21. Ndani ya mtiririko wa habari ya Injili hii, hakuna mtu aliyehukumiwa; hukumu ya wanadamuiliangukia juu ya mtu mmoja, "mara moja kwa wote." Mungu alitupa ushahidi wa hukumu ya haki ya wanadamu, kwa kumfufua Kristo kutoka katika wafu. Mdo 17:31; Rum.4:25. "Tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili." J.B. Phillips anatafsiri kwa kusomeka hivi: *"Ufahamu wetu kwa mtu hauwezi tenakujengwa juu ya maisha ya nje."* 2Kor.5:16. Mungu ametenda ndani yetu kile ambacho sheria haikuweza kutenda (hatukuweza kukamilisha haya kwa sheria, kwakuwa sheria ilituwekea mipaka ya mwili wetu; Mungu aliyotenda katika Kristo yanafungua namna mpya ya kutufikiria sisi, tuweze kujiona sasa katika utambulisho wa roho, tukiwekwa mbali na msukumo wa utawala wa mtu wa kale wa mwili wa dhambi). Kristo aliihukumu dhambi katika mwili, ili kwamba kama vile kutaka kwa sheria kutimizwe ndani yetu. Kristo alitia sahihi kibali cha kifo cha dhambi katika asili yetu." (Tafsiri ya Knox). Rum.8:3-5. Mtu anabaki kuwa hana uwezo kwa sababu zilizo kinyume cha ukweli, hivyo kujidanganya mwenyewe, na kubatilisha matokeo ya imani; hapo kunahitajika kuituliza dhamiri juu ya mambo ya roho. Kuwa na nia mbili kuhusu utambulisho wako wa kweli, kutakufanya uendelee kuchanganyikiwa na kukosa msimamo.

Yak.1:7,8. Sheria kamilifu ya uhuru, inakupa uhuru wa kuona hali yako halisi ya kweli, mbali na makanusho yote! Yak.1:25. “Enyi Wagalatia, kwanini mnajiruhusu wenyewe kuchukuliwa na udanganyifu wa elimu? Katika kupotezaimani ya kwanza yenye mgusowa kweli, unapoteza msingiwote ulioupata katika niayako! Kristo aliyesulibiwa, alihubiriwa kwa masimlizi ya maonyesho ya maana, ili kwamba, yaliyotokea kule katika historia, vile vile yalitokea ndani yako! Ukweli ulitangazwa kwa njia ambayo ulishuhudia kifo chake kama vile ni chako mwenyewe.” Gal.3:1. Imani sio fursa unayoipata; sio namna ya mshindo wa upofu gizani! Kwanza, Injili ni juu ya kitu unachokiona, kabla ya kitu unachokifanya; wala sio kufa kwako bali ni kutenda; ni kuona kwamba umekufa katika kifo chake; hakikaalikufa kifo chako! Rum.6:11; 1Kor.1:30. Nguvu za kidini nyingi sana hupotea juu yamajaribio yasiyo na sababu za maana kwa kufanya mambo ambayo tayari yalifanyika; kuwa vile ambavyo tayari ndivyo ulivyo. Kwa sababu ya ujinga, ukristo umekuwa sawa na Budddha; watu wamejiingiza kabisa katika mambo yasiyozaa, bali wanaendeleza juhudi za kifo. Unapogundua ukweli wa sura ya Mungu ndani yako, na uhalisi wa Kristo ndani yako, utampenda jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe! Kuona kunachochea hali ya kutenda; sheria ya ushirika ni kanuni ya imani. Rum. 3:27; Yak.1:25. Sheria ya imani ni sawa na sheria kamilifu ya uhuru. Pia, Paulo anayaita maisha haya kuwa ni sheria ya roho na sheria ya uzao mpya. Rum.8:2; Gal.6:15,16. Kamwe, ukweli hauwi chini ya vitisho; ujinga au makanushohaviwezi kufuta ukweli. Hatuwezi kufanya chochote dhidi ya kweli, ila kwa ajili ya kweli! 2Kor.13:8; Rum.3:3,4. Kukatishwa tamaa, kuvutwa mawazo, ujuzi binafsi aumashauri ya mtu mwingine yeyote, haviwezi kamwe kukushawishi kwenda kinyumena kweli! Hakuna haja ya kufanyiza vibaya au kuharibu neno la Mungu kwa kuyaminya mashauri ya Mungu na kuyaingiza





katika kukubaliana kama vile ndivyo ilivyokuwa, ili kumfanya Mungu akubaliane na mtu kuhusu kushindwa kwake. Ujuzi wa kibinadamu sio kipimo cha kweli. “Kwa maelezo wazi ya kweli, naishuhudia kila dhamiri ya mtu.” (Neno la Kigriki la dhamiri, *suneidesis,* kona -pamoja) na Kristo kama kuakisi kwa kioo kwa utambulisho wa kweli wa mtu; dai la dhamiri ya mtu ni dunia yote. 2Kor.3:18; 4:2. Paulo anaelewa kuwa mwanadamu ni wa asili ya dhamiri; kwa hiyo anashiriki majibu mema kwa hitaji la ukweli.

Mafundisho mengi yaliyo maarufu yamejengwa juu ya rejea za maandiko yanayotenga, nje ya hali ya mtiririko wa habari ya kazi ya Mungu ya ukombozi kama ilivyofunuliwa katika Kristo. Dhana yoyote inayoondoa habari njema ambayo Mungu aliileta kwa niaba ya mwanadamu katika Kristo itakuwa haina maana, bila kujali ni maandiko kiasi gani yanaweza kunukuliwa. Ukombozi ndiyo mazingira ya maandiko, hakuna hata historia yake au matengenezo ya desturi. Tafsiri nyingi kwamiaka mingi zimefanyizwa vibaya ili kuleta mashauri ya watu na tafsiri za kidesturi zaidi, kuliko ukweli wa kazi ya ukombozi wa mwanadamu iliyokamilika kutoka dhambini, na urejesho wa sura ya Mungu. Hisia za mtu za hatia na kupungukiwa zimeelezwa kwa nguvu kupitia vyuo vya kidini kwa miaka mingi. Mahekalu ya zamani mengi yenye utukufu ya wakatoliki, yanashuhudia juu ya ukweli huu. Uuzajiwa mamilioni ya hati za msamaha, daima ziliingiza mapato mengi katika miradi yamajengo haya. Hati hii ilikuwa kipande cha karatasi kilichotolewa kwa niaba ya Papaau askofu wa eneo kwa mamlaka ya kanisa, kikitoa ahadi zilizoandikwa za kupunguza muda wa kukaa tohorani! Uongo huu ulimpa mwanadamu uhuru kwa fedha ili kuendelea kutenda dhambi yoyote ya kutamanika bila kuwa na hisia za hatia, kwa kuwa alinunua unafuu fulani kwa ajili yake mwenyewe na kwa jamaa yake. Kukuza na kuuza hofu, kulifanyika kuwa

msisitizo mkubwa wa kanisa, hasa wakati makundi ya watu hawakuweza kuifikia Biblia ambayo ilikuwa imeandikwa katika lugha ambayo hakuwepo mtu wa kuelewa isipokuwa viongozi wa kanisa pekee. Inapotokea hatia, mashaka na hofu kwa ajili ya baadaye, daima mtuamekuwa ni mjinga kwa ajili ya adhabu. Si ajabu majengo makubwa na marefu katika siku za kale yaliyokuwa makanisa au mahekalu, na katika miji hiyo yote sikuza leo yamekuwa ni makampuni ya bima; yameendelea kuuza bidhaa ile ile, yaani, hofu. Mtu atalipa gharama yoyote kwa kufikiri kuwa atahisi kutulia kutokana na hatia au hofu. Miongoni mwa makanisa ya Kiprotestanti, ujumbe wa dhambi, jehanamu na hukumu ya milele, umekuwa ni mtindo maarufu wa kuwashawishi watu kufanya uamuzi kwa ajili ya Kristo. Mara nyingi inanishangaza jinsi watu wenye akili wanavyoweza kufikiria uhusiano wa upendo wa ndani wa kimbingu kati ya Mungu na mwanadamu, uliojengwa juu ya msingi wa hisia za kudumu za hofu, kushindwa, duni na hatia. Kwa namna fulani msisitizo juu ya kosa la Adamu na haliya dhambi ya mwanadamu, vinaonekana kuwa ndiyo mchanganyiko mkuu wa 'habari njema.' Wakati Injili ya kweli inafunua kuwa kipawa bure cha Mungu cha neema katika Kristo, kilifuta nguvu na maana ya dhambi. Ndiyo! "Mwivi huja ili kuiba, kuua na kuharibu, bali mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele!"

Yoh.10:10. Ndani ya Kristo, Mungu anafunua thamani ya kweli ya mtu. "Amenionyanisimwite mtu awaye yote najisi au mchafu!" Mdo 10:15,28; 1Yoh.5:9-11; 2Kor.5:16. Biblia nzima inamhusu Yesu, na yote yaliyo ya Yesu ni kwa ajili yetu! Kutokuamini kunaongeza ujinga au ufahamu mbaya na kumfanya mtu aendelee kunaswa katika akili duni na mashauri yake mwenyewe. Ujinga wa mtu haubadili ukweli kwamba wanadamu wote wanasimama wakiwa wameachiliwa





na kusamehewa mbele ya macho ya Mungu; hata hivyo, upinzani binafsi wa mtu kwa neno la kweli, iwe ni kwa ujinga, au ugumu wa kichwa chake na moyo wake, vinamwibia kufurahia faida za upendo wa Mungu, maisha yaliyojaa nuru. "Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye; maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali." 2Pet.1:3,9. Kutokuona kitu hakukifanyi kuwa hakipo. Ufahamuulioamshwa ni sawa na kutambua. Sura na chapa hubakia katika kuijua sarafu iliyopotea, haiwezi kamwe kupoteza utambulisho wa kweli au thamani. Marko 12:15-17; Mdo 17:27-29. Kama ilivyo katika sarafu, sura na jina la Mungu limechorwa katika kila mtu; Katika Kristo utambulisho wa kweli wa mtu ulitunzwa, ijapokuwa kulikuwa na anguko la Adamu. Upande wa kinyume wa mkanda unatunzamuda wa asili wa picha; hivyo Yesu hubakia kuwa chapa ya asili ya mtu.

"Watu humnena Mwana wa Adamu kuwa ni nani? Mwana wa Adamu ni Mwana wa Mungu." Math. 16:13-18. Swali hili linasisitiza umuhimu wa huduma ya Kristo; anatupa ufafanuzi sahihi wa asili ya kweli ya wanadamu na utambulisho wao wa kiroho. Kumwona yeye zaidi ya mawazo maarufu kutoka kwa mtu wa jinsi ya mwili,tunagundua uso wa uzao wetu kama katika kioo! 2Kor.5:16; Yak. 1:18,23. "Simoni mwana wa Yona, wewe ndiwe Petro." (Mwamba), mwana wa Petra (Mungu, Mwamba mkuu aliyekuzaa. Kumb.32:18). Katika lugha ya kisasa ya kompyuta, Mwamba unalingana na Mwendo Mgumu, hazina ya kumbukumbu za kudumu. Juu ya Mwamba huu, nitalijenga kanisa langu. *(ekklesia).* Kanisa ni neno lililobuniwa na watafsiri wa Biblia ya King James. Hakuna neno linaloshauri katika rejea za desturi zetu zinazojulikana, kuendelea na maana ya mtiririko wa habari wa kweli. Maneno mawili ya Kigriki yanaliunda neno la *ekklesia: ek,* neno la kutangulia lenye ishara yamwanzo; na neno *kaleo,*

lenye maana ya kukaribisha kwa sauti kuu, au kumpa mtu jina, au kumtambua mtu kwa jina, kumsalimu kwa jina. Hivi ndivyo hasa Yesu alivyofanya; alifunua mwanzo wa kweli wa mwanadamu (mwana wa Mungu) na alimpa Simoni jina jipya! Ni juu ya ufunuo wa utambulisho wa kweli kwamba Yesu analijenga ekklesia lake. Hili si jengo lililojengwa na wanadamu au shirika, bali mawe hai yaliyofunuliwa pamoja kama maskani ya Mungu duniani.

"Baba ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa." Ef. 3:15; Mal. 2:10,15; Is. 51:1. "Kutoka kwake tunachukua asili yetu." 1Kor.1:30. (Tafsiri ya Knox). "Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake akisema, 'Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu." Ebr.2:11,12. "Maana sisi sote tu watoto wake." Mdo 17:28. Yesu ni zaidi sana ya wayahudi. Yoh. 4:9,10. Yeye ni kipawa cha Mungu kinachohuisha chemchemi ya uzima (asili) ndani ya kila mmoja. "Yeye ni sura ya Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote." Kol.1:15. Vitu vyote vinashiriki uhalisi wao wa asili ndani yake. Yoh. 1:3. "Tukimtazama kama kwa kioo,tumebadilishwa ili kufanana naye." 2Kor.3:18. "Mungu alinitenga tangu tumboni mwa mama yangu, alipomfunua Mwana wake ndani yangu, ili niweze kumtangaza kwa mataifa! Gal.1:15,16. Tafsiri nyingi zinasema kuwa ni lazima Kristo ahubiriwe kwa mataifa. Kuna tofauti kubwa; ufunuo huu utainua dhana ya uinjilisti! "Hata imekuwa, tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili!" 2Kor. 5:14,16. Uzao bora wa Paulo katika mwili hauleti maana yoyote ya zaidi! Filipi 3:3-9. "Sasa haiwi tena Wayahudi na Mataifa, watumwa na watu huru, mwanaume au mwanamke, bali sisi sote tumekuwa mmoja katika Kristo." Gal.3:28. Ni wakati kwavitoto vya bata kujitambua vyenyewe katika kioo cha ukweli! *Ekklesia* ni mwangwi wa





sauti inayotangaza mwanzo wa utambulisho wa asili ya mtu. Maisha ya mwaminini barua hai inayoishuhudia kila dhamiri ya mtu, kujulikana na kusomwa na watu wote. 2Kor.2:2,3; 4:2. "Nalipewa neema hii ya kuwahubiri mataifa utajiri wake Kristo usiopimika, waijue siri iliyositirika tangu zamani zote, katika Mungu aliyeviumba vitu vyote, ili sasa kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namnanyingi, ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho. Hili lilikuwa kwa kadiri ya kusudi la milele, alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu." Ef.3:8-11. "Hatuwajibiki tena kuishi chini nya utawala wa asili ya dhambi, wala kumdanganya mtu yeyote kwa njia ya madanganyo na uongo; bali tunasimama na kutambulikanakikamilifu katika maarifa ya uumbaji mpya, sawasawa na mfano wa sura kamili ya muumbaji wetu." Kol. 3:9-11.

## MKAKATI WA MUNGU ASIA KATIKA MTU MMOJA

"Nisalimie Epaineto, mpenzi wangu, aliye malimbuko ya Asia kwa Kristo." Rum.16:5.Mungu anawaona wengi katika mmoja. Anaongea juu ya Ibrahimu, "Katika wewe mataifa yote watabarikiwa." Gal.3:8,9. Yeye ni Mungu "Ambaye hutaja yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako." (kwa sababu yapo) Rum.4:17. Sheria ilifunua jinsi kundi la wanadamu lilivyojumlishwa katika Adamu, na sasa kwa matokeo makubwa, Injili inafunua kuwa kundi lile lile la wanadamu, mmoja alisimama na kuhukumiwa katika Adamu, lilijumlishwa katika tendo la mtu mmoja lahaki. Rum. 5:15-19. "Miisho yote ya dunia imeuona wokovu wa Mungu wetu." Zab. 98:1-3. "Miisho yote ya dunia itakumbuka, na watu watamrejea Bwana; Jamaa zoteza mataifa watamsujudia. Wazao wake watamtumikia, zitasimliwa habari za Bwana,kwa kizazi kitakachokuja; nao watawahubiri watakaozaliwa haki yake, ya kwamba ndiye aliyeifanya." Zab. 22:27,30,31.

Habakuki anaiona haki kwa imani; anamwona mwanadamu amekumbatiwa na kurejeshwa kwa upendeleo bila hatia, kwa ajili ya matendo ya Mungu. Maoni haya yanatakiwa kuenezwa kwa usahihi mkubwa na uwazi, ili kwamba msomaji ayasome kwa haraka. Kwa kuwa dunia itajawa na maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari. Hab.2:2,4,14. Upinzani mkubwa sana hauwezi kubatilishashauku na furaha ambayo ni maarifa ya ukombozi ya kweli: "Maana mtini hautachanua maua, wala mizabibuni hamtakuwa na matunda; taabu ya mzeituni itakuwa bure, na mashamba hayatatoa chakula; zizini hatakuwa na kundi, wala vibandani hamtakuwa na kundi la ng'ombe; (hii inaonekana kama laana ya Kumb.28!)





lakini (kwa sababu ya haki kwa imani). Walakini nitamfurahia Bwana, nitamshangilia Mungu wa wokovu wangu. Yehova, aliye Bwana, ndiye nguvu zangu;yeye huifanya miguu yangu kuwa kama ya kulungu, naye ataniendesha katika mahali pangu palipoinuka!" Hab.3:17-19; Yak.1:2-4.

"Iandike njozi, ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji." Hab.2:2. "Kwa hiyo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangukatika siri yake Kristo." Ef.3:4. "Yafahamu sana hayo nisemayo, kwa maana Bwana atakupa akili katika mambo yote." 2Tim.2:7. "Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu (ujuzi sio mwalimu wa kweli), bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni." 1Kor.2:13. "Paulo alihubiri kwa namna ambayo wengi waliamini." Mdo 14:1. "Imani (ushawishi) huja kwa kusikia kunakotokana na ufunuo wa Kristo." Rum.10:17. "Lakini, kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, 'Naliamini, na kwasababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena." 2Kor.4:13. "Watu wale waliokwenda katika giza, wameona nuru kuu; wale waliokaa katika nchiya uvuli wa mauti, nuru imewaangaza. Umeliongeza taifa, umezidisha furaha yao; wanafurahi mbele zako, kama furaha ya wakati wa mavuno, kama watu wafurahivyo wagawanyapo nyara. Kwa maana umeivunja nira ya mzigo wake, na gongo la bega lake, na fimbo yake yeye aliyemwonea, kama katika siku ya Midiani (Mungualipotenda ushindi mkuu kwa Gidioni, pasipo silaha, bali tarumbeta tu na mianga ndani ya vyombo tupu vya udongo, katika siku ambayo walipunguzwa hesabu yao). Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi

yake na amani, hayatakuwa na mwisho kamwe. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo." Is.9:2-7. Juhudi ya Bwana inatofautiana kabisa na juhudi ya kidini kwa ajili ya Mungu. Juhudi ya Mungu inatiwa nguvu na ufunuo wa haki kwa imani. Hab.2:2,4.; Rum. 10:2,3. "Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako." Zab.2:8. Pembe za mwisho sana za dunia zitashuhudia wokovu wa Mungu ukija. Is.42:6,7; 52:7-10; 60:1-3,21,22; 61:1,2. Milango ya kuzimu haitauzuia wokovu wa kutambulikana kwa kweli kwa mtu. (*ha+ideis,* sio kuona, au ujinga wa kiroho) Math.16:13-18. Kama jiografia ingekuwa ni kipimo cha ukubwa wa wokovu, ndipo miisho ya dunia ingekuwa ndio mwisho wa jambo. Upana, urefu, kimo na kina cha upendo wa Kristo unaopita maarifa, unamtangazia kila mtu kuwa amejumlishwa katika mkutano mkubwa. Injilihii ni fungu la kila mtu. "Kwa kuwa mimi nawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote! Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." Luka 2:10,14.

Hatima ya habari njema ni kuupata ulimwengu. "Kila goti litapigwa, la vitu vya mbinguni na vya duniani; na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba." Filipi 2:10,11. Watu wote walifanyika wenye dhambi sanakwa njia ya anguko la mtu mmoja, Adamu; hawakuelewa haya mpaka sheria ilipolifunua; lakini watu wote walifanyika wenye haki sana kwa njia ya kifo cha mmoja na ufufuo; na bado hawaelewi mpaka wakati Injili inapoufunua. Rum.5:12,13; 7:7,13. Kutambua huku kunahimiza msukumo wa haraka kumwingizamtu mwingine katika uzima wake wa kuwa na umoja na Mungu! Ef.3:9; 2Kor.5:14-

21. "Kwa maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia." Mdo 4:20. Kutangaza habari za





furaha kunatoa maana ya uzima. "Lakini imo roho ndani ya mwanadamu, na pumzi za Mwenyezi huwapa akili. Kwa kuwa nimejaa maneno; roho iliyo ndani yangu hunihimiza. Tazama, tumbo langu ni kama divai iliyozibwa; kama viriba vipya li karibu na kupasuka. Nitanena ili nipate kutulia; nitafunua midomo yangu na kujibu." Ay.32:6-8,18-20. "Moyo wangu ukawa kama moto ndani yangu, na katika kuwaza kwangu moto ukawaka; nalisema kwa ulimi wangu!" Zab.39:3. "Wakaambiana, Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?" Luka 24:32. "Hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi; naushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo!" 1Yoh.1:3. Paulo anaongelea kuhusu nguvu ya ndani ambayo humhimiza kwa furahakuu na huruma, ili kumshawishi kila mtu kikamilifu katika ufunuo wa siri ya Mungu.Kol.1:24-29. Kumtazama kwetu kama kwa kioo, kunaongeza kiwango cha sauti yetu! Ufunuo wa neema unawasha moto ndani yetu! 1Kor.15:10. Imani hupata uvuvio wake katika maarifa ya ufunuo; Paulo anasema siri ya huduma yake, haikuwa katika ufasaha wa maneno au maneno ya ushawishi, bali katika maarifa ya imani. 2Kor.4:13; 11:6; 5:14; Ef..3:4; 1Kor.2:1-5. Huduma ya Paulo ilikuwa ya zaidi kuliko kuwa na uchaguzi wa manufaa tu; alisukumwa na upendo na furaha kwa sababu ya kile alichokijua kuwa ni kweli, katikati ya upinzani mkali. 2Kor.11:23-30; Filipi 4:11,12. Migogoro ya maisha na kupungukiwa havikuleta vitisho vyovyote vya kuharibu mguso wa upendo wa Mungu. Rum.8:37-39. Alihisi kuhojiwa na kudaiwa kuwavuta wote Wayunani wasomi, na makundi ya wasiosoma kujumlishwa kwao katika Kristo. Rum.1:5,14,15. Aliendelea kutenda kazi kwa mikono yake mwenyewe, bila kuweka mzigo wowote juu ya watu aliowahudumia, hata hivyo hakujulikana kamwe kama mtengenezaji wa hema; hata

utume wake haukuwa cheorasimi, bali kielelezo cha huruma yake; alisukumwa na neno kuwafanya watu wote waone. Mdo 18:3,5; 20:33; 1Thes.2:7-9; 4:11,12; 2Thes.3:6-13. Kwake uzima wa mwili ulimaanisha matunda ya kazi; kila jambo lililotokea kwake, lilikuwa kuendelezaInjili. Filipi 1:12,21-25. Wala hata kifungo cha gerezani hakikuzimisha au kuharibu maono yake; aliendelea kuliona neno kuwa halifungwi na mazingira yale. 2Tim.2:9. Alibakia kushawishika kikamilifu kuwa huduma yake isingekosa mafanikio kamwe au kuwa batili; wala asingekuwa mpiga ngumi asiye na malengo kwa kupiga hewani tu.1Kor.9:26 na sura ya 15:58. Alielewa thamani ya kila mtu, na alijua kuwa, ufunguo wa kumfikia mtu wa pili, ni kumfikia huyu mmoja. 2Kor.5:16; 10:12-16; 2Tim.2:2. Kamwe Yesu hakumshusha mtu bila kujali sifa yake; alifika mji wa Sikari kwa njia yamwanamke mmoja. Yoh.4:40-42. Katika Marko 5:19 na 20, anaiona miji kumi katika ushuhuda wa mtu mmoja! (Dekapoli = miji 10.) Filipo anaongozwa na Roho katika njia ya upweke ili kumleta Mkushi mmoja kwa Kristo; kuna bara ndani ya mtubinafsi! Mdo 8:26-40.

Paulo hakuongozwa kwa milango iliyofunguliwa, bali kwa kujua kuwa daima Munguanatuongoza kwa ushindi, na kupitia sisi anaeneza harufu ya kumjua yeye kila mahali. 2Kor.2:12-14. Mungu aliona zaidi ndani ya Gidioni kuliko vile Gidioni alivyojiona mwenyewe. Kabla hajakutana na neno la Bwana, maisha yake yalishushwa na kuokolewa tu. Waam.6:11,12,14-16. Mungu analiangalia neno lake ili alitimize! Yer.1:5-12. Yeremia anaona mti wa mlozi; jina la kiebrania kwa mti wamlozi ni mti ulioamka, kwa kuwa ni mti wa kwanza kuchanua na kuzaa matunda, wakati mingine yote bado inalala!"Hamsemi ninyi, bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno. Mimi naliwatuma myavune yale msiyoyataabikia; wengine





walitaabika, nanyi mmeingia katika taabu yao!" Yoh.4:35,38. "Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo 'mpatanishwe na Mungu. Nasi tukitenda kazi pamoja naye, twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure.' Tazama wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndio sasa." 2Kor.5:18-21; 6:1.

Haki kwa imani inasema, "Mungu ametenda; Kwa Mungu mmekuwa katika Kristo, amelitenda, tunaingia katika kazi yake iliyokamilika, tunaingia katika raha yake (tunda la kazi yake), mahali tunapokoma kufanya matendo yetu wenyewe! "Leo ukiisikia sauti yake, usifanye moyo wako kuwa mgumu." Ebr.4:2,7,10; Is.26:12. Utiiwetu na imani imekuwa badala ya imani yake. Ndiyo aliyoyafanya na tunaamini kuwa yeye huhuisha matendo na imani yetu. Watu wasiosoma, watu wa kawaida ndio waliupindua ulimwengu wao. Mdo 1:5-8; 4:13; 8:5-7,26,27,40; 10:1,5,28; 17:6; 1Kor.1:26-31; Ebr.12:1-3. "Bado kuna ardhi ya kuimiliki." Yosh.13:1. Watu wote wa Asia walilisikia neno kwa muda wa miaka miwili kama matunda ya huduma iliyoelekezwa kutoka shule moja! Mdo 19:8-11. "Panda juu ya mlima mrefu wewe uhubiriye Yerusalemu habari njema, paza sauti kwa nguvu." Is.40:9. Fikiria lugha ya mjumbe arudiye kutoka uwanja wa vita akiwa na habari za furaha za ushindi! "Jinsiilivyo mizuri juu ya milima, miguu yake aletaye habari njema; Yeye aitangazaye amani, aletaye habari njema ya mambo mema, yeye autangazaye wokovu!" Is.52:7.

(Maandiko yamenukuliwa: Biblia ya RSV, isipokuwa imeonyeshwa vinginevyo, na piatafsiri huru kutoka maneno ya asili, na mwandishi)

*Cover design by ELMO SWART*

Vitabu vingine kuendeleza kiini kimoja:

MUNGU ANAKUAMINI WEWE (Pia Ki- Afrikaana, Ki-Rusi na Ki-Venda).

ILITENDEKA! (Ki-Afrikaana).

SIRI IMEFUNULIWA (Ki-Afrikaana, Ki-Rusi). JINSI YA UPENDO WAKE.

SHANGWE YA URAFIKI.

MAAJABU KATIKA KRISTO. Andre Rabe.

Title of the book: KUMBATIO

LA KI-MUNGU

© Copyright 2010 - Francois du Toit. The detailed copyright notice can be viewed here: http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Your_Right_to_Copy

(You may freely copy, but not sell, make any changes or claim/ imply ownership ofany portion or the whole of the text)

Note, all material on the mirrorword.net site is FREE of charge:

1. Read how the Mirror revelation - knowing Jesus as in a mirror - is totallytransforming people and nations: http://www.mirrorword.net/About_Us/Testimonies

2. The MirrorWord bible translation (a definite MUST HAVE) - the best grace-basedtranslation of the bible from the original languages!
http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/MirrorWordBible
*(Knowing Jesus as in a mirror and the significance of the cross is the key tounderstanding the bible)*

3. Subscribe yourself or others (they can unsubscribe) for a short & powerful dailyrevelation sent to your email address: http://www.mirrorword.net/Daily_Thoughts

4. Audio and video teachings of wordschools and selected teachings:
http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Audio
http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Video

5. Various books and shorter teachings to download and read:
http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Books_Magazines
http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Articles

6. Study material for groups/individuals and books and a lot more: www.scribepublishing.co.za

7. The material is being translated in many other languages (you're welcome to help!) http://www.mirrorword.net/1Other_Languages

8. Join the rich and wonderful grace discussions online: www.facebook.com/mirror.reflection.net www.facebook.com/francois.toit

9. Join the online school of grace - amazing place where people's lives are beingtransformed in a friendly environment: www.schoolofgrace.net (or email andre.rabe@gmail.com).

10. Check out the following addresses for more of the Mirror revelation: www.scribepublishing.co.za www.hearhim.net
More links: http://www.mirrorword.net/About_Us/Links

11. How you can get involved with biblestudy groups etc.: http://www.mirrorword.net/Get_Involved
Enjoy - you were made for it!

12. If you desire to make donations towards the ministry to help others hear thegood news... We are a registered Non-profit organisation: http://www.mirrorword.net/Get_Involved